**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

---

*Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

**MEI, 2018**

## YALIYOMO


1.0 **UTANGULIZI** ........ 1

2.0 **UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018** ........ 2

2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ........ 3

2.1.1 Miradi iliyokaguliwa na Kamati ........ 3

3.0 **MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018** ........ 7

4.0 **SEKTA NDOGO YA GESI NA MIRADI YA MAFUTA NCHINI** ........ 9

5.0 **HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI** ........ 12

6.0 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018** ........ 14

6.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 ........ 14

6.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina ........ 16

6.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ........ 20

7.0 **UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2018/2019** ........ **21**

7.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ........ 21

7.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato ........ 22

7.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ........ 24

8.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........ 24

9.0 **HITIMISHO** ........ 29

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yote ya kisera yanayotekelezwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati katika Wizara kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka yameelekezwa katika Fasili ya 7(1), Kamati imetekeleza ipasavyo majukumu hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matakwa ya kanuni tajwa, Kamati ilifanya vikao kadhaa kwa lengo la kupokea na

kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Pia Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Lengo la ukaguzi huo ni kujionea hali halisi ya matumizi ya fedha za miradi zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka husika.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati, katika Mikoa ya Mara, Shinyanga, Tabora na Singida.

Aidha, Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa fedha na ambayo haikutengewa fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2017/2018. Miradi iliyokaguliwa ni hii ifuatayo:-

i) Miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Mara.
ii) Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv Iringa – Shinyanga (Backbone), mkoani Shinyanga.
iii) Miradi ya umeme Vijijini, Mkoa wa Shinyanga.

iv) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).

v) Miradi ya Umeme vijijini mkoa wa Singida.

vi) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, mkoani Singida.

## 2.1 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

### 2.1.1 Miradi iliyokaguliwa na Kamati

i) **Miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Mara**

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa ambayo miradi ya umeme vijijini Awamu ya Tatu inatekelezwa, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Mradi huu unahusu miradi midogo ya Densification, Uendelezaji wa Grid ya Taifa (Mizunguko ya I na II) na Mradi mdogo wa maeneo nje ya grid (off-grid).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Vijiji viwili vya wilaya ya Butiama ambavyo ni Busegwe na Muriaza. Vijiji hivi viko katika mradi wa Densification. Kamati ilibaini changamoto kubwa ya ushirikishwaji mdogo wa wananchi pamoja na Viongozi wa maeneo husika na hivyo kusababisha maeneo muhimu na yenye watu wengi kutofikiwa umeme kama inavyotakiwa. Aidha,

changamoto hiyo imesababisha maeneo mengi katika vitongoji na vijiji kurukwa wakati wa upelekaji wa umeme huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini kuwa mashine Humba zilizofungwa kwaajili ya kusambaza umeme zina uwezo mdogo ikilinganishwa na mahitaji ya eneo husika, hali hiyo inapelekea maeneo hayo kutokuwa na umeme wa uhakika.

ii) **Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv Iringa – Shinyanga (Backbone), mkoani Shinyanga**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mradi wa REA awamu ya tatu mkoa wa Shinyanga umepata miradi miwili, ambayo ni mradi wa REA – III (grid extension) na mradi wa kuvipatia huduma ya umeme vijiji vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovolti 400 (VEI/BTIP). Aidha, Kamati ilitembelea vijiji viwili vya Negezi na Bulimba vinavyopatiwa umeme kupitia Mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa REA awamu ya tatu kwa mkoa wa Shinyanga unajumuisha ujenzi wa km 669.4 za laini za msongo wa kilovoti 33, ujenzi wa km 453 za laini za msongo wa volti 400, ufungaji wa transfoma 201.

Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa ya jumla ya **shilingi bilioni 33.054**.

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Shinyanga pia umepata mradi wa laini kubwa ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 400 yenye urefu wa kilomita 670 kutoka mkoani Iringa kupitia mikoa ya Dodoma na Singida hadi kwenye kituo cha kupooza umeme cha Ibadakuli. Mradi huu uligharimu jumla ya **dola milioni 120 takribani kiasi cha shilingi 268,800,000,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto kubwa inayoikabili miradi hii ni Vijiji vingi bado havijapata umeme kwa awamu ya kwanza ya mradi, hasa maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri za miji ya Kahama, Kishapu na Shinyanga vijijini.

iii) **Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi ya REA, inayotekelezwa katika Wilaya ya Nzega, kijiji cha Idala pamoja na kijiji cha Iborogero wilayani, Igunga.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu pia Mkoa ulipata mradi wa kupeleka

umeme kwenye vijiji 12 vilivyoko pembezoni mwa mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme (400KV) kwa wilaya ya Igunga katika mkoa wa Tabora na wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.

Pamoja na utekelezaji unaoendelea katika miradi hii, Kamati iliona changamoto ya maeneo mengi ya vijiji na vitongoji kukosa umeme. Aidha, utekelezaji ulionekana ni wa kusuasua, na sababu zikianishwa ni ukosefu wa Fedha. Hata hivyo, bado Viongozi na Wananchi hawashirikishwi katika uainishaji wa maeneo hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kurukwa kwa maeneo mengi.

iv) **Miradi ya Umeme vijijini mkoa wa Singida pamoja na Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, mkoani Singida**

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Singida unapata umeme kutoka Gridi ya Taifa kupitia njia kuu za kusafirisha umeme za msongo wa Kv 400, katika mradi wa REA awamu ya tatu mkoa Singida umepata miradi 2, ambayo ni mradi wa REA – III (Grid Extension) na mradi wa kuvipitia huduma ya umeme vijijini vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kv 400.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea ofisi ya Tanesco ya mkoa Singida na kuona kituo cha kupoza umeme cha

TANESCO kupitia mradi huu wa msongo wa umeme wa KV400. Aidha, Kamati ilitembelea kijiji cha kisaki na kujionea hali ya upatikanaji wa umeme.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** pamoja na miradi inayoendelea kwa mkoa huu bado kuna changamoto ya vijiji kukosa umeme. Aidha, maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida bado hayajafikiwa na huduma ya umeme. Vilevile, kuna maeneo ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani hapo hayajapatiwa umeme kama vile mradi wa umwagiliaji maji mkoani hapo.

## 3.0 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

a) Utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini awamu ya tatu uzingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa maeneo wanaohusika.

b) Miradi ya umeme vijijini bado inakabidiliwa na changamoto kubwa ya upelekwaji wa Fedha kwa wakati, hali hiyo inapeleka wakandarasi kuchelewa

kutekeleza miradi kikamilifu na kwa wakati. Hivyo basi, kamati inaitaka Serikali kupeleka fedha kwa wakati kwakuwa fedha hizi zina wigo na ni tozo za wananchi

c) Katika kutekeleza miradi hii ya umeme vijijini, bado maeneo mengi ya vijiji na vitongoji yanarukwa, Kamati inaishauri Serikali, kuainisha maeneo kwa kuwashirikisha viongozi pamoja na kuongeza wigo (scope) kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii, ili wigo uwe wa kukidhi maeneo mengi ya vijiji. Mfano kijiji cha Nyabange Wilaya ya Butiama ni nyumba nne tu zimeunganishwa na umeme na mkandarasi ameshakamilisha kazi yake.

d) Miradi ya umeme vijijini bado inakabiliwa na changamoto ya mashine Humba zisizo kidhi viwango vya matakwa ya maeneo. Mashine Humba (Transformer) zinazofungwa hazina ubora wenye kuaminika. Kamati inashauri Serikali kufanya ukaguzi wa Mashine humba kabla wakandarasi hawajazifunga katika maeneo.

e) Kamati inapendekeza pia wananchi kulipwa fidia zao kwa wakati katika maeneo ambayo miradi mbalimbali inatekelezwa.

f) Kamati inaendelea kushauri Serikali kupeleka umeme katika maeneo ya Miji na Halmashauri, Aidha, kipaumbele cha kupeleka umeme kwa kuzingatia zaidi maeneo ya miji ambayo shughuli mbalimbali za uzalishaji na za kiuchumi zinapotekelezwa. Mfano katika Mkoa wa Singida kuna Mradi wa maji /umwagiliaji haujaunganisha na umeme.

## 4.0 **SEKTA NDOGO YA GESI NA MIRADI YA MAFUTA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza sekta ya Mafuta na Gesi. Mnyororo huu wa thamani unahusisha mkondo wa juu (utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi), mkondo wa kati (uchakataji na usafirishaji wa gesi na mafuta) pamoja na mkondo wa chini (usambazaji wa mafuta na gesi kwa watuamiaji).

**Mheshimiwa Spika,** tangu kugundulika kwa Gesi Asilia nchini jumla ya Viwanda 41 vimeunganishwa tayari katika mpango wa matumizi ya gesi asilia; kati ya hivyo viwanda vinne vimesimamisha uzalishaji na viwanda 37 vinaendelea kutumia gesi asilia.

Aidha, kwa Mwaka wa fedha 2017/18 takwimu za matumizi ya Bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam kupitia Somanga Fungu linauwezo wa kupitisha wastani wa futi za ujazo milioni 175 kwa siku, ikilinganishwa futi za ujazo milioni 145 kwa siku kwa mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa uzalishaji wa Gesi asilia kwa siku imepelekea ongezeko la uzalishaji wa umeme wa MW 697 unaokwenda kwenye gridi ya Taifa kwa mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na kasi ya ukuzaji wa soko la matumizi ya Gesi asilia majumbani na viwandani. Pamoja na uwepo wa Gesi asilia ya kutosha nchini na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi toka Mtwara hadi Dar es Salaam; Idadi ya watumiaji wa Gesi asilia waliounganishwa kwa matumizi ya Viwandani na majumbani nchini siyo ya kuridhisha. **Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali itoe fedha za kutosha ili kujenga miundo mbinu ya kusambaza gesi hiyo.**

**Mheshimiwa Spika**, mahusiano ya wadau katika sekta yoyote ile ni jambo la muhimu sana, wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) katika kipindi cha robo Mwaka kwa Mwaka wa fedha 2017/18, Kamati haikuridhishwa na mahusiano ya ubia ya kuendeleza miradi ya gesi asilia inayotekelezwa kati ya TPDC,

PAN AFRICAN ENERGY, SONGAS pamoja na TANESCO. Ili mahusiano hayo yawe na tija kwa Taifa, Kamati iliona ni vema Bunge lako tukufu lifuatilie na kujua maendeleo ya Mikataba na mahusiano baina ya wabia hao katika kuendeleza miradi hii ya Gesi.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inakupongeza sana wewe binafsi kwa kuchukua hatua za haraka kuunda kamati Maalum ya kufanya mapitio ya uwekezaji uliofanyika katika sekta ya gesi nchini na kutoa mapendekezo kuhusu namna bora ya kuendeleza miradi ya Gesi asilia nchini .**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na umuhimu wa nchi kuwa na ghala la kuhifadhia mafuta ya dharura (Strategic Petroleum Reserve),**Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa ghala la kuhifadhia mafuta ya dharura ya Taifa. Mradi huu una manufaa makubwa kwa nchi na utasaidia uwepo wa mafuta ya dharula kwa nchi wakati wote.**

**Mheshimiwa Spika,** Pia Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zinazoendelea katika utekelezaji wa mradi wa Bomba la kusafirishia mafuta ghafi la kutoka Hoima-Uganga hadi Tanga-Tanzania. Mradi huu una manufaa makubwa kwa Taifa kwakuwa mafuta haya yatauzwa katika masoko ya Kimataifa

hivyo kuliongezea Taifa mapato. Pamoja na manufaa makubwa ya mradi huu kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Seriakali kuangalia kwa umakini matumizi ya fedha za mradi huu kwa kuwa asilimia kubwa ya utekelezaji wa mradi huu ipo upande wetu.

## 5.0 HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya upatikanaji wa umeme nchini inaendelea kuimarika hadi sasa **MW 1,347.51** zimeshaingizwa kwenye gridi ya Taifa, umeme huo unatokana na vyanzo mbalimbali kama vile nguvu za maji **MW 567.70,** Gesi asilia **MW 698.91**, **Mafuta MW 70.4** na Biomass **MW 10.50.**

Matumizi ya juu kabisa yaliyowahi kufikiwa na nchini yetu ni **MW 1,051.27** kimsingi matumizi hayo ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji ya umeme katika maeneo yote yaliyo nje ya gridi, Kamati inashauri Wizara kuendelea na jitihada za kuhakikisha mikoa yote inaingia kwenye gridi ya Taifa ili umeme wote unaozalishwa kutoka kwenye vyanzo vyote uweze kutumiwa na mikoa yote nchini ili kuondoa dhana ya kuwa nchi yetu ina umeme wa ziada kwenye gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi pekee katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuwa na mitambo ya kisasa ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia (combined cycle). Mitambo hii ina uwezo wa kuchoma gesi na kuzalisha umeme pia mitambo hiyo ina uwezo wa kuzalisha megawati nyingine kwa kutumia mvuke. **Aidha, Ni matarajio ya Kamati kuwa uwepo wa Gesi asilia ya kutosha nchini, pamoja na mitambo ya kisasa ni ishara tosha kuwa nchi yetu inapaswa kuwa na umeme wa uhakika na wakutosheleza mahitaji ya nchi yetu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara ya Nishati katika kuwekeza kwenye miradi mipya ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji wa umeme kama vile Stiglers gorge, miradi ya umeme wa jotoardhi na mingine, bado maeneo mbalimbali ya nchi yanakabiliwa na tatizo la kukosa umeme wa uhakika, umeme unaokatika mara kwa mara, hali inayopelekea kukwamisha shughuli mbalimbali za uzalishaji na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ukarabati wa miundo mbinu ya kusafirishia umeme pamoja na vituo vya kufua umeme nchini zipelekwe zote na kwa wakati kwa shirika la TANESCO ili kuweza kutekeleza jukumu la ukarabati wa miundombinu na vituo hivyo. Hali hii itasaidia sana kuondoa kero kubwa ya ukatikaji wa umeme**

**inayosababishwa na uchakavu wa miundo mbinu katika maeneo mbalimbali hapa nchini.**

## 6.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

b) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na;

c) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

### 6.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2018 Wizara ya Nishati ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 216.20** sawa na **asilimia 57.3** ya lengo lililokusudiwa la **Shilingi bilioni 377.46** hadi kufikia robo tatu ya mwaka 2017/18. Kamati inaona kwa mwenendo huu wa ukusanyaji mapato, na kwakuzingatia muda uliobaki kabla ya kufikia mwisho wa

mwaka; upo uwezekano mkubwa kwa Wizara kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuongeza juhudi za ukusanyaji katika kipindi kilichobaki.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa makusanyo ya Mapato kuanzia Julai 2017 hadi mwezi Februari, 2018 unapatikana kwenye kielelezo Na. 01 cha Taarifa hii.

**Kielelezo Na. 01**

| CHANZO CHA MAPATO | BAJETI YA 2017/18 | LENGO LA MAKUSANYO HADI ROBO YA TATU YA 2017/18 (SH. BILIONI) | MAKUSANYO HADI MWISHONI MWA MWEZI FEBRUARI, 2018 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya Gesi Asilia | 477,361,499,676 | 358,021,124,757 | 188,336,575,696 | **52.6** |
| Mapato mengine | 11,725,135,724 | 8,793,851,793 | 19,787,668,054 | **225** |
| Ubia | 2,864,538,296 | 2,148,403,722 | 0 | **-** |
| Mrabaha na Gawio la Faida ya Gesi | 11,339,000,000 | 8,504,250,000 | 8,084,618,029 | **95** |
| **Jumla (Sh.)** | **503,290,173,696** | **377,467,630,272** | **216,208,861,779** | **57.3** |

6.2 **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (Fungu 58) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 998.34** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2018 iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 259.80,** sawa na **asilimia 34.7** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako ilikuwa ni **Shilingi bilioni 938.63,** sawa na **asilimia 94** ya bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hadi kufikia Februari 2018 **Shilingi Bilioni 228.66** zilikuwa zimetolewa, sawa na **asilimia 39.94 tu** ya fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa **Shilingi bilioni 763.30** sawa na **asilimia 81.3** ya Bajeti yote ya maendeleo ni Fedha za ndani na **Shilingi bilioni 175.33** sawa na **asilimia 18.7** ya bajeti hiyo ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 756.76** sawa na **asilimia 80.6** ya bajeti yote ya maendeleo zimeelekezwa kwa ajili ya miradi ya kimkakati (Strategic Projects) ambayo ni pamoja na mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini (REA), mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV400 wa

Singida–Arusha–Namanga utakaounganisha nchi ya Tanzania na Kenya na mradi wa Kinyerezi I *Extension* MW 85.


Kwa upande wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi bilioni 28.83** na hadi kufikia Februari, 2018 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 13.94**, sawa na **asilimia 64.52** ya fedha zilizoidhinishwa.

Ufafanuzi zaidi kuhusu uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana hadi Machi, 2017 ni kama unavyoonekana kupitia Kielelezo Na. 2 katika taarifa hii.

**Kielelezo Na. 2**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2017/2018 | | | FEDHA ILIYOPATIKANA HADI MACHI,2018 | |
|---|---|---|---|---|
| **UFAFANUZI** | **KIASI** | **ASILIMIA** | **KIASI** | **ASILIMIA** |
| **JUMLA KUU** | Bil 998.34 | 100 | Bil 259.80 | 34.7 |
| **FEDHA ZA MAENDELEO** | Bil 938.63 | 94 | Bil 229.50 | 32.6 |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | Bil 59.7 | 6 | Bil 30.30 | 67.68 |

***CHANZO:*** *Taarifa ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18*.




**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji malipo ya wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya REA. Hali hii inatokana na uanzishwaji wa utaratibu mpya wa uidhinishaji malipo unaozuia REA kuidhinisha malipo moja kwa moja kutoka kwenye akaunti ya mfuko wa Nishati Vijijini. Kwa mujibu wa utaratibu mpya, REA inalazimika kuwasilisha maombi Wizara ya Nishati ndipo maombi hayo yapelekwe Wizara ya Fedha na Mipango.

Kamati ilibaini kuwa licha ya wakandarasi kuwasilisha maombi ya malipo ya awali tangu mwezi Agosti mwaka 2017, ulipaji wa madai hayo ulichukua takriban miezi minne kwa baadhi ya wakandarasi; na wakandarasi wengine hadi mwezi machi 2018 malipo yao yalikuwa bado hayajaidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Wakandarasi wanaotekeleza miradi hii waliwasilisha maombi yao ya malipo toka mwezi Agosti, 2017, hata hivyo; hadi kufikia mwezi machi 2018 takriban miezi 10 tangu kuingiwa kwa mikataba ambayo utekelezaji wake ni wa miaka miwili, bado ufunguzi wa Hati za Muamana (***Letters of Credit***) ambao ni takwa la kimkataba kuwawezesha wakandarasi kununua vifaa ulikuwa haujafanyika.

Ucheleweshaji huu wa ufunguzi wa Hati za Muamana utasababisha kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa miradi; pamoja na kutotimia kwa lengo la kuvifikishia umeme vijiji vyote nchini kabla ya mwaka 2020.

Licha ya REA na TANESCO kufanya uhakiki wa kina wa malipo hayo kwa kufuata kanuni na Sheria ya Nishati Vijijini; utaratibu wa sasa wa uidhinishaji malipo unaitaka Wizara ya Fedha nayo kuyafanya uhakiki madai ya malipo hayo.

**Kamati imebaini kuwa mfumo huo mpya wa uhakiki wa malipo umekuwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa malipo kwa Wakandarasi; hivyo REA kukiuka makubaliano ya mikataba waliyosaini kati yao na wakandarasi. Hivyo basi; Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo mzuri utakaofupisha utaratibu huu usio wa lazima ili miradi ya REA iweze**

**kutekelezwa kwa wakati, na vile vile kuiepusha Serikali na hasara ya kulazimika kulipa fidia kwa wakandarasi kutokana na REA kukiuka makubaliano ya mikataba.**

6.3 **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2017/18, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 iliyoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

a) Utekelezaji wa miradi ya REA bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya maeneo mengi kuachwa/kurukwa katika vijiji na vitongoji pamoja na Viongozi na Wananchi kutoshirikishwa vya kutosha katika uainishaji wa maeneo.

b) Serikali bado haitengi na kupeleka bajeti ya kutosha kuiwezesha TPDC kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa. Mfano dhahiri ni kusuasua katika kutekeleza miradi ya kusambaza gesi katika

mikoa ya Dar Es Salaam na mikoa mingine; hususan kuwekeza katika miundombinu ya kusambaza gesi kwa watumiaji.

c) Serikali bado hailiwezeshi vya kutosha Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) kwa kulipatia Fedha za kutosha kutelekeza majukumu yake. Kama vile ukarabati wa Miundo mbinu na vituo vya kufua umeme.

d) Miradi ya Joto ardhi bado imeshindwa kutekelezwa kutokana na kutokupelekewa fedha. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni **asilimia 0.17** tu ya fedha za miradi ya maendeleo ndiyo iliyopelekwa kwa taasisi ya TGDC.

## 7.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA (FUNGU 58) MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 7.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2018/19 Wizara itatekeleza na kusimamia Malengo Makuu Sita (6) yafuatayo:-

i) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;
iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;
iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;
v) Kutekeleza kwa ufanisi mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waarithika.

**Mheshimiwa Spika,** malengo haya yakitekelezwa vizuri yatatimiza azma ya Wizara ya kuhakikisha kuwa rasilimali za Nishati zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi, kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya Watanzania.

## 7.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka 2018/19 ni **shilingi 394,450,860,000**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **shilingi 394,440,858,600** zitakusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **shilingi 10,002,000**

zitakusanywa kupitia shughuli za utawala. Kiasi hiki ni pungufu kwa **shilingi 108,839,313,096** ikilinganishwa na mapato yaliyotarajiwa kukusanywa mwaka 2017/18.

**Kamati inaamini kuwa kadirio hili ni la chini na kwamba Wizara inao uwezo wa kukusanya zaidi endapo itaweka mikakati madhubuti kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa vyanzo na rasilimali zilizopo.**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Wizara ya Nishati inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni 1,692,286,014,000** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 998,337,759,500** kwa mwaka 2017/18 kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, sawa na ongezeko la **asilimia 69.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2018/19 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 1,665,141,000,000** sawa na **asilimia 98.4** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya Fedha za ndani iliyotengwa kwajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 1,489,741,000,000** sawa na **asilimia 89.5** ya bajeti ya maendeleo sawa na **asilimia 99** ya bajeti yote ya fedha za ndani imetengwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati.

## 7.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya matumizi ya kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2018/19 ni **shilingi 27,145,014,000** sawa na **asilimia 1.6** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya Fedha hizo **shilingi 15,025,821,000** ni kwajili ya matumizi mengineyo (O.C) na **shilingi 12,119,193,000** ni kwajili ya mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

# 8.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa fedha 2017/18 na makadirio na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/19, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

8.1 Bunge linaidhinisha Fedha za miradi ya maendeleo kama Wizara inavyoomba kwa kila Mwaka wa fedha husika , **Hivyo basi Kamati inashauri Serikali kupeleka Fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati, Kutopatikana kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo hali inayopelekea miradi kuzorota na washauri elekezi kutokulipwa fedha za kutekeleza miradi.**

8.2 **Kwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo wa kusuasua hususani miradi ya REA; ambapo hadi kufika tarehe 5 Mei, 2018 ni vijiji 4,730 vimefikiwa na miundo mbinu ya umeme kati ya vijiji 12,268 vya Tanzania bara, Kamati inaona kuwa azma ya kuvifikishia vijiji vyote miundo mbinu ya umeme haitatimia ifikipa 2021.**

8.3 Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi mipya ya usafirishaji na usambazaji umeme ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo, kuja na mkakati maalum wa kuunganisha mikoa yote iliyo nje ya gridi ya Taifa hususani Kigoma, Katavi, Lindi, Mtwara, Kagera na Rukwa.

8.4 Upatikanaji wa umeme nchini bado ni changamoto kubwa katika maeneo mengi kutokana na miundo mbinu mibovu hali inayopelekea kukwama kwa shughuli nyingi za uzalishaji hasa za viwanda, **Kamati inashauri Serikali kutoa fedha za kutosha kukarabati miundo mbinu ya umeme ili kupunguza adha kwa wananchi na kuondokana na tatizo la umeme kukatika mara kwa mara.**

8.5 **Serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa majadiliano ya uwekezaji wa mradi wa LNG ili kukwepa tishio la kutekwa kwa soko la biashara ya gesi na nchi nyingine.**

8.6 Kamati inaendelea kusisitiza kwa serikali kuwekeza katika vyanzo vingine vya kuzalisha Nishati mbadala, Aidha, **kuwekeza zaidi katika nishati jadidifu (*renewable energy*) ambayo uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa mazingira, mfano uzalishaji wa umeme wa upepo katika maeneo ya Singida, Makambako na Same yenye upepo wa kutosha.**

8.7 Serikali ihakikishe TANESCO inajielekeza kwenyeb matumizi ya teknolojia ya kisasa yatakayoiwezesha kutokuzima umeme pindi inapofanya matengenezo ya Mitambo.

8.8 Kamati inaishauri Serikali kuja na mkakati wa kulipa madeni ya Taasisi inazosimamia na kuonesha jitihada za dhati katika kulipa wazabuni wanaozidai taasisi hizi. Mfano Hadi kufikia Februari 2018, Wazabuni mbalimbali walikuwa wanaidai TANESCO jumla ya **Shilingi bilioni 969**.

8.9 Kamati inaishauri Serikali kuendelea Kuimarisha doria katika njia za umeme pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme

ili kupunguza tatizo la wizi wa umeme na vishoka ambao wamekua wakiiba umeme.

8.10 **Kamati inaendelea kuishauri na kusisitiza kwa Serikali kushirikisha wananchi pamoja na viongozi wao wakati wa kuainisha maeneo ya kutekeleza miradi ya REA, kwa kufanya hivyo, maeneo mengi ya vijiji na vitongoji hasa yale ya kijamii yatapata huduma ya Nishati hii muhimu.**

8.11 **Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia ubora wa vifaa hasa mashine Humba '(*Transformer)*' zinazofungwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu.**

8.12 Katika kuhamasisha uwazi na uwajibikaji wa rasilimali za mafuta na gesi Asilia, **Serikali inapaswa kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya manufaa ya rasilimali hizi za mafuta na gesi asilia na faida zake kama taifa katika utumiaji wa rasilimali hizi. Aidha, manufaa yauwepo wa rasilimali hizi yanapaswa kuonekana kwa wananchi.**

8.13 **Kamati inaiushauri Serikali kulipa fidia kwa wakati wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, mfano miradi ya Gesi Asilia *LNG***

**mkoani Lindi, pamoja na wananchi wa Igunga waliopisha mradi wa ujenzi wa kusafirisha umeme Kv400 Singida- Arusha.**

8.14 **Serikali inapaswa kutafuta fursa zaidi za masomo kwa vijana kwajili ya kuendeleza taaluma mbalimbali kuhusiana na masuala ya uendelezaji ya Nishati kama vile jotoardhi. Kusomesha vijana katika kuendeleza taaluma hizi kutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la uhaba wa wataalam pamoja na kuongeza soko la ajira nchini tena wenye ujuzi stahiki.**

8.15 **Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuendeleza kampuni yake ya Tanzania Concrete Poles Manufacturing company limited (TCPM) katika utengenezaji wa nguzo za zege. Na kwakuwa hata kuingia ubia na Wawekezaji wengine utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Hivyo basi, ili kuharakisha matumizi ya nguzo hizo katika miradi inayoendelea hususani Miradi ya REA Kamati inashauri Serikali kuharakisha utekelezaji na uendelezaji wa kampuni hiyo kwa kuipatia mtaji, vilevile kutoa fursa kwa kampuni ambazo zinazalisha nguzo hapa nchini.**

## 9.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara, katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi**.**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt Medard Matogolo Kalemani, (Mb), Mhe. Subira Khamis Mgalu, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye Hansard:-

1. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb

5. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
6. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
7. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
8. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
9. Mhe. Ussi Salim Pondeza, Mb
10. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
11. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
12. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
13. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
14. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
15. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Ajari Rashid Akbar, Mb
18. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb
19. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb
20. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
22. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
23. Mhe., Mohamed Ally Kessy, Mb
24. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
25. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto,

Makatibu wa Kamati Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja, pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndg. Grace Mwenye, kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya; sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo ni **Shilingi 1,692,286,014,000.**

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
24 Mei, 2018